**KISWAHILI**

**028**

**14/11/2019 8:30 AM – 11:30 AM**

Rwanda Education Board

# MTIHANI WA TAIFA KWA SHULE ZA SEKONDARI, 2019

**SOMO: KISWAHILI**

**MICHEPUO:**

- **LITERATURE IN ENGLISH -KISWAHILI-KINYARWANDA (LKK)**
- **LITERATURE IN ENGLISH- KISWAHILI- FRENCH (LKF)**

## MUDA: Masaa matatu

**MAELEZO:**

1) Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.

2) Andika majina yako na nambari yako kwenye karatasi ya majibu kama vilivyoandikwa kwenye karatasi ya kujiandikisha.

3) Mtihani huu ambao una sehemu ya I, II, III na ya IV una maswali 23 kwa alama 100:

**Sehemu ya I**: Jibu maswali yote **(alama 30)**

**Sehemu ya II**: Jibu maswali yote **(alama 30)**

**Sehemu ya III**: Jibu maswali yote **(alama 25)**

**Sehemu ya IV**: Jibu swali moja **(alama 15)**

4) Andika vizuri nambari ya kila swali.

5) Mwandiko wako usomeke vizuri.

6) Tumia kalamu ya bluu.

**Soma habari ifuatayo kisha uyajibu maswali yatakayofuata**

Isipokuwa hakuna anayeweza kukanusha kauli kuwa mtoto ni kipawa chake Mungu muumba wetu, lakini hatuna budi kukubali kwamba kitu chochote kisichotunzwa vyema na kupaliliwa ipasavyo, huwa hakina manufaa sana. Hali kadhalika, ili jambo au mradi wowote ule kufanikiwa ni sharti kuwe na sera na mpango madhubuti na maongozi muafaka juu yake. Vipengele vyote vya maendeleo ya taifa kama elimu, afya, uchukuzi, nyumba, kilimo, na huduma nyinginezo hutegemea sana viwango vya ongezeko la watu nchini.

Mnamo mwaka wa 1974, katika kongamano la kimataifa la Umoja wa Mataifa lilitambua mpango wa uzazi katika jamii zote kama mojawapo ya haki za mume na mke na jamii nzima kwa jumla. Katika azimio lililopitishwa kwenye kongamano hilo, imeelezwa kwamba watu wote wana uhuru na haki za kujiamulia kwa busara na hiari ya watoto wanaowataka na mpango wa kuachana kwa watoto wale kadiri wanavyozaliwa.

Isitoshe, watu wote wana haki ya kupata habari na elimu au maarifa ya kuwawezesha kutekeleza mpango wao wa uzazi. Kutekelezwa kwa haki hii lazima kutilie maanani maslahi ya wazazi na watoto wao kuhusu afya na wajibu wao wote kwa aila na jamii zao.

Katika mataifa mengi ya Kiafrika, ingawa dhana ya kupanga uzazi si jambo linalotiliwa mashaka sana kama hapo zamani, bado watu wengi hasa katika sehemu za mashambani hawapendi kutumia njia za kisasa za kupanga uzazi. Isitoshe, baadhi yao hawatumii njia yoyote ya kupangia uzazi. Viongozi wengi wa Serikali na Mashirika wamo mbioni kuwahimiza, kuwaelimisha na kuwatangazia raia haja na umuhimu wa kutekeleza mpango wa uzazi . Lakini licha ya juhudi kubwa inayofanywa na matumizi ya hazina za taifa na misaada ya kigeni, tunafahamishwa kuwa ni chini ya asilimia kumi tu ya wanawake walioitikia mwito huu katika bara letu la Afrika.

Kwa hivyo, ni wazi kuwa matumizi ya njia za kitaalamu za kisasa hayajakubalika miongoni mwa Waafrika wengi. Je, ni nini kinachosababisha kusita huku kutumia njia hizi au hata kukubali kabisa kwamba kila mmoja ana wajibu wa kupanga jamii yake? Kwa sasa tutasema tu kuwa ingawa kuna mbinu nyingi za Kimagharibi za kupanga uzazi, hazikuletwa hapa Afrika kwa kuambatana na mila, mienendo, itikadi na imani zetu kama Waafrika. Kwa mfano katika jamii nyingi za Kiafrila, ni desturi kwamba mashauri yanayohusu uzazi hujadiliwa faraghani baina ya mume na mke.

Mathalani, tukiangalia hali ilivyo katika nchi tofauti barani Afrika, tutaona kuwa ni dhahiri mpango wa uzazi kwa kutumia njia za kigeni ni jambo lililohusishwa na utamaduni na mila za mataifa ya Kimagharibi. Tangu Serikali zianzishe jitihada za kueneza elimu ya mpango wa uzazi kutokea miaka ya sitini, ni wanaume wachache hata miongoni mwa wale wenye elimu ya kisasa waliopata

kuunga mkono hasa kwa vitendo. Baadhi yao, huwasukumia kina mama wajibu wote wa kupanga uzazi na isitoshe, wengi wao huwakataza katakata wake zao kushiriki katika mpango wenyewe.

Serikali kupitia kwa wizara ya Afya na mashirika zinajitahidi kufa na kupona usiku na mchana kuhakikisha kuwa kila mwananchi anaelewa na kuthamini umuhimu wa kupata watoto kwa kuambatanisha au kulingana na uwezo wake wa kuwatunza na kuwamudu.

Maongozi yetu ya kidemokrasia yanamruhusu kila mmoja kujiamulia maisha yake ya baadaye bila kuingiliwa kisheria. Hii ni kinyume na hali ilivyo katika mataifa mengine mengi ambayo yameweka sheria nyingi kuzuia ongezeko la watu. Kwa mfano, hapa kwetu hatuna idadi iliyowekwa kisheria ya watoto kwa mume na mke wala hapana mtu anayeshurutishwa kutumia njia yoyote ya kupanga uzazi. Hali kadhalika, sheria zetu haziruhusu mtu yeyote kuharibu mimba ama kuiavya kwa njia yoyote.

Je, kwa jumla ni mambo gani yanayofanya upangaji wa uzazi kuwa jambo muhimu na la dharura kubwa? Sio tu kwamba dunia imejaa maafa na misukosuko ya kila aina bali pia majanga ya kimaumbile kama vile mitetemeko ya ardhi, mifuriko, mipigo ya radi, ukosefu wa mvua na kuharibiwa kwa mimea ya chakula na hali mbaya ya anga ni mambo yaliyoenea sana. Je, hii ni sababu ya kutosha ya kuendelea kazaana kwa wingi? La hasha.

**SEHEMU YA I. UFAHAMU (Alama 30)**

Jibu maswali yafuatayo kulingana na habari ambayo umeisoma hapa juu

1) Andika kichwa kifaacho kwa habari hii **(alama 2)**

2) Taja angalau vipengele 4 vya maendeleo ya taifa **(alama 4)**

3) Ni nini kilichotambulika katika Kongamano la kimataifa lililofanyika mwaka 1974? **(alama 2)**

4) Ni nani anaye neno la mwisho kuhusu uamuzi wa mpango wa uzazi? **(alama 1)**

5) Ni nani anaye haki ya kupata maarifa ya kumwezesha kupanga uzazi? **(alama 1)**

6) Kutokana na habari, katika bara letu la Afrika ni kiwango gani cha wanawake walioitikia mpango wa uzazi? **(alama 1)**

7) Unafikiri ni kwa sababu gani viongozi wengi wa Serikali na Mashirika huwaelimisha raia kuhusu mpango wa uzazi? **(alama 5)**

8) Kwa sababu gani Waafrika wengi husita katika harakati za kupanga uzazi? **(alama 5)**

9) Mume na mke wana wajibu gani kuhusu jamii yao? **(alama 4)**

10) Toa muhtasari wa habari hii uliyoisoma hapa juu. Kati ya mistari 5 na 7. **(alama 5)**

**SEHEMU YA II: MATUMIZI YA LUGHA NA SARUFI (alama 30)**

11) Tunga sentensi yako mwenyewe kwa kutumia maneno yafuatayo: **(alama 6)**

(a) manufaa

(b) kutekeleza

(c) wajibu

12) Eleza kazi zinazofanywa na watu wafuatao **(alama 4)**

(a) Mvuvi

(b) Mwashi

13) Andika sentensi hizi kwa kutumia kinyume cha kitenzi kilichoandikwa kwa herufi mlazo. **(alama 3)**

(a) Mtoto na mama yake *wanapanda* mlima

(b) Mshtakiwa *alikana* mashtaka yote

(c) Alishangaa kwa *kufeli* mtihani wake

14) Tia sentensi zifuatazo katika usemi taarifa: **(alama 4)**

(a) " kesho tutaenda sokoni" Mama alimwambia mtoto wake

(b) "Mko wanafunzi wangapi hapa darasani?" mwalimu alimuuliza kiranja.

15) Eleza maana ya maneno yafuatayo kuhusu uhusiano wa kifamilia **(alama 4)**

(a) Shangazi

(b) Binamu

16) Ondoa " amba" katika sentensi zinazofuata bila kubadili maana yake **(alama 4)**

(a) Wanafunzi ambao watashinda vizuri watatunukiwa

(b) Shamba ambalo linapaliliwa vizuri litatoa mazao mengi

(c) Gazeti ambalo ulilisoma lina habari zinazofurahisha

(d) Kiti ambacho kinavunjika kilikuwa kinakaliwa na watu wengi

17) Jaza nafasi tupu kwa kutumia maneno yafuatayo: **(alama 5)**

**uhusiano; habari; lugha; kupeleka; Lengo; uelewano; jamii; msingi; kudhoofisha; chombo**

Maana ya lugha

Lugha ni ... cha kupashana .... Mtu mmoja ana habari fulani, anaipeleka habari hiyo kwa mtu wa pili kwa kutumia maneno yaani .... Huko ... habari toka mtu mmoja mpaka kwa mtu mwingine, ndiko kunafanya kuwepo na kuwasiliana.

Lugha ni chombo cha kuwasiliana kati ya watu. ... la lugha katika kuwasiliana ni kujenga ... na kuelewana; japo mara nyingine kuwasiliana kunaweza kusababisha kutoelewana na ... uhusiano. Katika lengo lake la kuleta ... katika jamii, huo uelewano huleta amani. Amani ni ... mmoja muhimu wa maendeleo kwa ....

**SEHEMU YA III: FASIHI (alama 25)**

18) Eleza methali zifuatazo na utoe hali tunapoweza kutumia kila moja **(alama 6)**

(a) Ukistaajabu ya Mussa utaona ya Firauni

(b) Patiliza udongo ungali maji.

(c) Ng'ombe akivunjika guu malishoni hurudi zizini kusaidiwa.

19) Kwa kutoa mifano kadhaa, eleza namna fasihi inavyoweza kuburudisha jamii. **(alama 5)**

20) Andika methali yoyote inayoelimisha watu kutoa malezi bora. **(alama 3)**

21) Toa mfano wa riwaya uliyojifunza na muhtasari wake katika mistari kati ya 7 na 10. **(alama 6)**

22) Fani na maudhui havitengani bali hutegemeana ili kazi ya fasihi iweze kuwa bora zaidi. Jadili **(alama 5)**

**SEHEMU YA IV: UTUNGAJI (alama 15)**

23) Chagua swali moja kati ya haya yafuatayo chini uandike maneno kati ya 200 nan 250 **(alama 15)**

(a) " Wewe ni Mkuu wa Idara ya Utamaduni na Huduma za jamii wilayani na umealikwa kuhutubia vijana kuhusu miradi yao ya kujiendeleza. Iandike hotuba yako."

(b) " Mtoto ni mtoto awe wa kike au wa kiume." Tunga insha kuonyesha ukweli wa wazo hili.

UKURASA TUPU

UKURASA TUPU